BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Nne – Tarehe 20 Februari, 2023
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii:

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii ya mwaka 2022/2023.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

58. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Hali ya kuongezeka kwa matukio ya kihalifu nchini imepelekea kuongeza hofu kwa wananchi. Uhakika na usalama wa watu na mali zao na uhifadhi wa maadili na silka za Mzanzibari, kwa kiasi kikubwa vimekosekana hasa kwa kukithiri kwa matukio hayo. Aidha, kuna kila dalili kwamba watu wamekuwa wakiingia Zanzibar bila ya utaratibu na mpangilio maalum, hali ambayo inapelekea kushindwa kudhibiti uhalifu na kuuweka usalama wa jamii katika hali hatarishi na isiyo na muamana.

(a) Je, Serikali inajua ni watu wangapi kwa wastani na kutoka wapi wanaoingia Zanzibar na wangapi wanaotoka, angalau kwa kila mwaka.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa dharura na wa muda mrefu wa kuhakikisha kwamba inapambana na uhalifu ulio kithiri katika jamii, ikiwemo kuondoa wimbi la ukabaji, ubakaji, wizi na matukio mengine ya jinai.

(c) Je, Serikali inatumia mfumo gani wa kuonesha takwimu sahihi na za uhakika za idadi ya watu wanaoingia na kutoka Zanzibar.

**<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>**

95. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Katika shehia ya Kengeja eneo la Mbuyuni, lipo diko ambalo linakodishwa na Baraza la Mji Mkoani.

(a) Je, kuna asilimia yoyote ya malipo ambayo wanapewa wananchi kutokana na mapato yanayotokana na diko hilo.

(b) Na kama wanapewa ni nani anayekabidhiwa fedha hizo.

(c) Na kama hawapewi, Je, wananchi wanafaidika vipi na fedha zinazotoka katika eneo hili.

**<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>**

59. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Katika kuitekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020-2025 kuna baadhi ya changamoto zinazokabili utekelezaji wake, hasa kwa baadhi ya ahadi zilizomo katika Ilani hiyo zinahitaji zaidi utashi wa kisiasa na maamuzi ya kiutawala ambayo hayahitaji fedha au huhitaji fedha nyingi ili kutekelezwa. Hata hivyo, hakuna mpango makhsusi ulioainishwa wa jinsi ya kupata fedha za kuigharamia Ilani ya CCM katika miradi mikubwa.

(a) Je, ni mpango upi wa uhakika wa Serikali wa kupata fedha kwa ajili ya kuleta mapinduzi katika kilimo, uvuvi na uwekezaji wa viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, uvuvi na mifugo.

(b) Je, ni mpango upi wa uhakika wa Serikali wa kupata fedha kwa ajili ya kuendeleza sekta ya mafuta na gesi asilia Zanzibar kama sekta mkakati, kuendeleza sekta ya utalii, na kuiwezesha Zanzibar kujitegemea kinishati

(Energy Independence).

<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>

78. MHESHIMIWA PANYA ALI ABDALLA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa kuwa Serikali inajitahidi katika kukuza lugha ya Kiswahili kwa kuandaa makongamano mbali mbali baina yetu na nchi za jirani. Na kwa kuwa wenzetu wa Tanzania Bara wameona umuhimu wa kuwaendeleza wataalamu wa lugha ya Kiswahili na wanatoa mikopo kwa ajili ya kuwashajihisha wataalamu hao kuongeza elimu zao.

Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mpango gani wa kuwaendeleza wataalamu wa lugha hiyo hapa nchini.

<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>

35. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembe Samaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

(a) Serikali ina mkakati gani wa kumalizia “Hall” la skuli ya Sekondari Kiembesamaki lililojengwa kupitia michango ya wazazi na wadau tofauti wa elimu.

(b) Baada kumalizika kwa “Hall” hilo, Je, Serikali italitumia kwa shughuli zipi ukiacha mbali matumizi ya wanafunzi kulitumia kwa kufanyia mitihani yao.

<u>Wizara ya Afya:</u>

39. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa Wizara ya Afya imekuwa na jukumu kubwa la kusimamia na kuboresha huduma za afya Zanzibar.

(a) Je, kuna mpango gani wa kuanzisha utengenezaji wa dawa na baadhi ya vifaa tiba mfano ‘gloves’ na ‘drips’ ambazo mali ghafi zake zinapatikana ndani ya Tanzania, ili kuepuka changamoto ikiwemo gharama za uingizaji kutoka nje ya nchi.

(b) Je, Wizara imefanya mazungumzo na viwanda vya utengenezaji wa vifaa tiba kuona namna ya kuanzishwa

kwake hapa Zanzibar.

**<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>**

111. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Itakumbukwa kuwa jengo letu la Kihistoria la Beit Al Jaib liliporomoka na badala yake kufanyiwa matengenezo. Wakati wa matengenezo hayo wako ndugu zetu wapatao sita waliathirika ambapo wawili kati yao walifariki dunia na wengine kubakia vilema.

(a) Je, Serikali haioni aibu kuona kuwa hadi leo hii waathirika hawa hawajapewa hata kifutia machozi.

(b) Kwa kuwa jambo hili limeshakuwa la siku nyingi tena, je ni ipi kauli ya Serikali juu ya malipo ya watu wetu hawa.

**<u>Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:</u>**

130. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Falsafa ya Uchumi wa Buluu inahitaji kupewa kipaumbele kikubwa hususan katika kupata wataalamu waliobobea katika fani hii.

(a) Je, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ina mikakati gani ya kutoa kipaumbele kwa kuwapatia mikopo nafuu wanafunzi wanaojitolea kusomea fani ya Uchumi wa Buluu kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

(b) Mpaka sasa Wizara ya Uchumi wa Buluu ina wataalamu mahsusi wangapi katika fani hii na nini matarajio yao.

(c) Ni kwa kiasi gani wataalamu hawa wamekuwa chachu ya kuleta ufanisi hususani katika sekta ya uvuvi kwa ujumla wake.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

6. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

   Daraja la Uzi katika jimbo la Mwanakwerekwe, limekuwa ni kivuko kikubwa na kiunganishi muhimu sana kwa wananchi wanaopita kwa miguu pamoja na vyombo vyao.

   Je, Wizara yako, ipo tayari kushirikiana na viongozi na wananchi wa jimbo la Mwanakwerekwe kulifanyia ukarabati daraja hilo na vivuko vyengine kwenye jimbo la Mwanakwerekwe.

11. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

    Ni jambo la kupongezwa kwamba Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi iliweka uzio katika Uwanja wa Ndege wa Pemba. Hata hivyo, inasikitisha kwamba kuna taarifa za kuaminika zinazothibitisha kwamba mkandarasi wa ujenzi huo, hadi leo bado hajalipwa fedha zake na Serikali.

    (a) Je, ujenzi wa uzio wa Uwanja wa Ndege wa Pemba uligharimu kiasi gani kama gharama ya ukandarasi na ushauri elekezi.

    (b) Je, ni kiasi gani cha fedha kimelipwa na kiasi gani hakijalipwa na lini kitalipwa.

    (c) Je, ni ipi sababu ya Serikali ya kuchelewesha malipo ya kazi hiyo na kwa mwaka wa fedha 2022/2023 deni hilo limekusudiwa kulipwa kwa programu ipi.

84. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

    Kumekuwa na mazoea na imekuwa ndio utaratibu wa wamiliki wa vyombo kutoza gharama za (kuchaji) matoroli ya mizigo nchini pindi boti inapofunga nanga, jambo ambalo linasababisha mrundikano wa watu.

    Je, utaratibu huu wa kutoza gharama hizo unatekelezwa kwa sheria ipi.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

16. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Katika kipindi hiki cha karibuni, zao la nazi limethibitika kukosekana sana na kupelekea nazi moja tena ndogo ya wastani kuuzwa zaidi ya shilingi elfu mbili za kitanzania.

(a) Je, kuna uhusiano wowote wa kukatwa kwa minazi mikubwa ya asili na kukosekana kwa nazi hapa Zanzibar.

(b) Je, ni mikakati gani ya dharura na ile ya muda mrefu ambayo Wizara inaitekeleza katika kulinusuru zao la nazi lisipotee kabisa.

(c) Je, takwimu zinazungumziaje juu ya uhaba huo kwa hivi sasa katika nchi yetu.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

75. MHESHIMIWA SALMA MUSSA BILAL (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa kiasi kikubwa wananchi wa Zanzibar wamekuwa wakikumbwa na tatizo la kukatika kwa umeme katika Jiji la Zanzibar licha ya huduma hiyo kuboreshwa. Hali hii inawachosha wananchi na kupelekea vifaa vya majumbani kuungua.

(a) Je, Serikali kupitia Wizara yako inawaambia nini wananchi wanaokumbwa na tatizo hili kila mara.

(b) Ni sababu gani hadi leo umeme wa Zanzibar haupo “standard” kulingana na nchi ya wenzetu.

(c) Je, ni hatua gani zinazochukuliwa kukabiliana na tatizo hili licha ya kuwa kuna ongezeko la matumizi ya umeme kila siku ndani ya visiwa vyetu.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

114. MHESHIMIWA HABIB ALI MOHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kwa kuwa uzalishaji wa mafuta ya makonyo unaendelea katika kiwanda cha makonyo.

Je, ni kiasi gani cha mafuta ya makonyo kimezalishwa kuanzia mwezi wa Julai 2022 hadi Disemba, 2022.

## III. HOJA ZA KAMATI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii ya mwaka 2022/2023.

**Zanzibar,**
**20 Februari, 2023.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**